# Hali ya Uhamiaji na Ustahiki wa Mpango wa Upanuzi wa Medicaid

NCMEDICAID FOR MORE PEOPLE

**NC Medicaid sasa inagharamia watu wenye umri wa miaka 19 hadi 64 wenye mapato ya juu. Unaweza kupata bima ya huduma ya afya kupitia mpango wa Medicaid hata kama hukuhitimiza vigezo vya ustahiki hapo awali. Mpango wa Medicaid hugharamia ziara za kumuona daktari, vipimo vya kila mwaka, huduma ya dharura, huduma ya meno, afya ya akili na zaidi – kwa gharama ndogo au bila ya gharama yoyote kwako.**

**Kuanzia Disemba tarehe 1, 2023, watu wengi wanaweza kupata bima ya huduma ya afya kupitia NC Medicaid ikiwa:**

- **Unaishi North Carolina**
- **Una umri wa miaka 19 hadi 64**
- **Wewe ni raia (baadhi ya watu ambao si raia wa Marekani wanaweza pia kupata bima ya huduma ya afya kupitia mpango wa Medicaid).**
- Na ikiwa **mapato ya kila mwezi ya kaya yako** yanalingana na orodha ya mapato kwenye chati iliyopo hapa chini:

| Idadi ya Wanakaya | Mapato ya Kila Mwezi ya mwaka wa 2025* |
|---|---|
| Watu Wazima ambao ni Waseja | Yasiyozidi $1,800 |
| Familia ya watu 2 | $2,433 au chini |
| Familia ya watu 3 | $3,065 au chini |
| Familia ya watu 4 | $3,698 au chini |
| Familia ya watu 5 | Yasiyozidi $4,340 |

**Vikomo vya mapato husasishwa kila mwaka.*

Baadhi ya watu ambao si raia wa Marekani wanaweza kupata bima ya afya kupitia mpango wa Medicaid. Ili kustahiki ni sharti uishi North Carolina na usiwe raia wa Marekani aliyetimiza vigezo vya hali ya uhamiaji. Watu wengi katika kitengo hiki sharti wasubiri miaka mitano kabla ya kutuma ombi kwa mpango wa Medicaid (ingawa kuna hali maalumu zinazoruhusiwa, kama ilivyoelezwa hapa chini).

Hali inayotimiza vigezo vya uhamiaji ni pamoja na:

- Wakazi wa Kudumu Kisheria (LPR/Mtu mwenye Kadi ya Kijani)
- Wahamiaji waliopewa hifadhi
- Wakimbizi
- Wakimbizi wa mpango maalumu wa kutoka Kuba/Haiti
- Mkazi nchini Marekani chini ya masharti maalum kwa angalau mwaka mmoja
- Mkimbizi aliyeruhusiwa kuingia nchini ya masharti maalum kabla ya mwaka wa 1980
- Watu ambao si raia wa Marekani, wenzi katika ndoa, watoto au wazazi ambao wamedhulumiwa ("Kupigwa" inamaanisha kuwa mtu ambaye amedhulumiwa na mwanafamilia.)
- Wahasiriwa wa usafirishaji haramu wa binadamu na wenzi wao, mtoto wao, ndugu au mzazi au watu binafsi walio na ombi linalosubiri kuidhinishwa kwa ajili ya kupewa viza ya mhasiriwa wa usafirishaji haramu wa binadamu.
- Idhini ya kuzuia kurudishwa nchini mwako kwa sababu za kiusalama (hali Mahususi iliyo sawa na hali ya mtu anayetafuta hifadhi)
- Wanafamilia wasio raia wa marekani wanaotoka kwa kabila la Wahindi linalotambuliwa na serikali kuu au Muhindi wa Marekani aliyezaliwa nchini Kanada
- Raia wa Visiwa vya Marshall, Mikronesia na Palau ambao wanaishi katika mojawapo ya majimbo au maeneo yaliyo chini ya utawala wa Marekani (wanaojulikana kama wahamiaji wa Compact of Free Association au COFA)

Baadhi ya watu ambao si raia wa Marekani katika orodha iliyopo hapo juu SI lazima wasubiri hadi miaka 5 ili kustahiki kuandikishwa kwenye mpango wa Medicaid, wakiwemo wanawake wajawazito, watoto walio na umri wa chini ya miaka 19, wahamiaji waliopewa hifadhi, wakimbizi, wahasiriwa wa usafirishaji haramu wa binadamu, Wakimbizi wa mpango maalum wa kutoka Kuba-Haiti na watu ambao sasa wana hali ya LPR na ambao hapo awali walikuwa wahamiaji waliopewa hifadhi, wakimbizi, wahasiriwa wa usafirishaji haramu wa binadamu, au wakimbizi kutoka Kuba-Haiti. Pia, watu wote ambao si raia wa Marekani kutoka kwenye orodha iliyopo hapo juu ambao wana uhusiano na jeshi kama vile wanajeshi wastaafu, wanajeshi wanaohudumu(na wenzi na watoto wao) hawatalazimika kusubiri miaka mitano ili kustahiki kuandikishwa kwa mpango wa Medicaid. Watu wengine wote ambao si raia katika orodha iliyopo hapo juu ni sharti wasubiri miaka mitano kutoka wakati wa kukuwa katika hali ya uhamiaji iliyotimiza vigezo ili kustahiki kuandikishwa kwa Mpango wa Medicaid.

### Ikiwa hakuna hali yoyote ya uhamiaji iliyoidhinishwa ambayo imeorodheshwa hapo juu inakuhusu:

Ikiwa wewe si raia wa Marekani au hauko katika kategoria hizi za uhamiaji, lakini unaweza kutimiza vigezo vya kupata NC Medicaid, bado unaweza kutuma maombi ya kupata bima ya kugharamia huduma ya hali ya dharura ambayo ni pamoja na:

- **Malipo ya gharama za kujifungua.** Pata bima ya gharama za matibabu wakati wa uchungu wa uzazi na kujifungua. Unaweza kutuma maombi baada ya hadi miezi mitatu baada ya kujifungua.
- **Ulipaji wa ada za huduma za dharura.** Pata bima ya kugharamia matibabu ya kutibu hali ya dharura, kama vile mshtuko wa moyo, kiharusi au ajali mbaya. Unaweza kutuma maombihadi miezi mitatu baada ya kutokea kwa hali hiyoya dharura.

**Ili kupata bima hii ya kugharamia huduma ya hali ya dharura, tuma maombi ya kujiandikisha kwenye NC Medicaid kama mtu wa kawaida** — lakini hauhitaji kuonyesha hati au kujibu maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji.

### Je, maelezo yangu yanaweza kushirikiwa kwa ajili ya utekelezaji wa sheria za uhamiaji?

Mpango wa Medicaid hautoi taarifa yoyote kwa asasi za kutekeleza sheria au Idara ya Uhamiaji na Utekelezaji wa Sheria za Forodha (ICE). Taarifa zako zitahifadhiwa kwa faragha na siri. Hii inajumuisha taarifa za wanafamilia wako walio na hali tofauti za uhamiaji. Taarifa zako haziwezi kutumika kwa madhumuni ya utekelezaji wa wa sheria za uhamiaji.

**Unahitaji tu kutoa taarifa kuhusu hali ya uhamiaji au nambari za Ustawi wa Jamii za wanafamilia wanaotuma maombi ya kujiandikisha kwa bima.** Kwa mfano, mzazi ambaye ni mhamiaji asiyestahiki anaweza kutuma maombi kwa niaba ya mtoto anayestahiki. Mzazi hatahitaji kutoa taarifa kuhusu hali yake ya uhamiaji. Kwa maelezo zaidi kuhusu ustahiki wa bima ya afya kwa wahamiaji, soma brosha hii kutoka kwa NC Justice Center.

### Je, utumaji wa maombi au upokeaji wa msaada wa Medicaid unachukuliwa kuwa utegemezi wa msaada kutoka kwa umma?

Hapana. Utumaji wa maombi au upokeaji wa msaada wa Medicaid hakumfanyi mtu kuwa "mtegemezi wa msaada kutoka kwa umma ". Haitaathiri hali yako ya uhamiaji au maombi yako ya uhamiaji. Ni mafao matatu pekee yanazingatiwa kuwa mabaya ikiwa unatuma maombi ya uhamiaji: Mpango wa Mafao wa Serikali Kuu Unaotoa Msaada wa Kifedha kwa Walemavu wenye Mapato ya Chini(SSI), Mpango wa Mafao wa Serikali kuu Unaotoa Msaada wa Muda kwa Familia Zenye Uhitaji (TANF), na Mpango wa Medicaid ikiwa tu utatumika kugharamia gharama za kulazwa hospitalini kwa muda mrefu au huduma za utunzaji wa nyumbani.

Mipango mingine yote ya mafao na afya ni salama kutumia na hazina athari yoyote kwa ombi la uhamiaji unalowasilisha. Kwa maelezo zaidi kuhusu utegemezi wa msaada kutoka kwa umma, soma kipeperushi hiki chenye maelezo kutoka kwa NC Justice Center .

### Je, wahamiaji ambao taarifa zao hazijarekodiwa wanastahiki kujiandikisha kwa mpango wa Medicaid?

Wahamiaji ambao taarifa zao hazijarekodiwa wanastahiki kuwa na mpango wa Medicaid wa kugharamia huduma za hali ya dharura. Hata hivyo, wahamiaji ambao taarifa zao hazijarekodiwa hawastahiki kujiandikisha katika bima ya huduma ya afya inayofadhiliwa na serikali kuu ikijumuisha mipango kamili ya Medicaid, CHIP, au Medicare, au kununua bima kupitia mpango wa Health Care Marketplace (ACA). Wahamiaji ambao taarifa zao hazijarekodiwa wanaweza tu kustahiki kuwa kwenye mpango wa Medicaid wa kugharamia huduma za dharura au huduma za leba na kujifungua.

### Je, mpango wa Medicaid wa kugharamia huduma za hali ya dharura ni nini na ni nani anayestahiki?

Kila mtu anaweza kustahiki mpango wa Medicaid wa kugharamia hali ya dharura ilmradi tu anakidhi vigezo vya mapato na masharti ya ustahiki wa kuishi katika jimbo la North Carolina (toa hati za uthibitisho kuwa anaishi North Carolina, kama vile kitambulisho cha picha kilicho na anwani yako, stakabadhi za bili ya matumizi, stakabadhi za mkataba wa ukodishaji au hati za kazi). Watu wasio raia wa Marekani ambao taarifa zao hazijarekodiwa na ambao hawastahiki bima ya huduma kamili ya afya chini ya mpango wa Medicaid wanaweza kupata bima ya kugharamia huduma za matibabu ya hali ya dharura. North Carolina ina mkandarasi wa ukaguzi wa matibabu ya hali ya dharura wa jimbo ambaye anabaini ikiwa tukio hilo linakidhi vigezo vya kuwa hali ya dharura ya matibabu na kubainisha tarehe ambazo mpango wa Medicaid unaweza kugharamia. Bima ya huduma itatumika kwa tarehe fulani, kuanzia tarehe ambayo hali ya dharura ya matibabu hutokea na kuhitimika tarehe ambayo hali hiyo ya dharura ya matibabu imedhibitiwa. Kwa mfano, mtu anapopata ajali ya gari na kupelekwa kwa chumba cha dharura (ER) au wanawake wanaojifungua na hawana bima.

### Je, ni nani anayestahiki mpango wa Medicaid katika kaya yenye wanakaya walio na hali tofauti za uhamiaji?

Watumaji maombi wote sharti wakidhi masharti ya makazi na mapato ya jimbo. Wazazi wanaweza kutuma maombi kwa ajili yao wenyewe na/au kwa niaba ya watoto wao.

- Wazazi ambao hawana stakabadhi halali zinazoonyesha hali ya uhamiaji, wanastahiki tu huduma za hali ya dharura pekee.
- Watoto wao wanaweza kustahiki mpango wa Medicaid kikamilifu ikiwa wana stakabadhi zinazofaa ambazo zinaonyesha hali ya uhamiaji. Hii ni kweli hata ikiwa wazazi wao hawana stakabadhi zinazofaa ambazo zinaonyesha hali ya uhamiaji.

Ikiwa ni mwanafamilia mmoja tu anayetuma maombi ya bima au msaada, ni mtumaji/watumaji maombi pekee ndio wanaopaswa kutoa stakabadhi zenye taarifa ya hali ya uhamiaji au nambari yao ya ustawi wa jamii. Wanafamilia wengine ambao hawatumi maombi si lazima watoe stakabadhi zenye taarifa ya hali ya uhamiaji.

### Je, ni taarifa gani ambayo wazazi ambao taarifa zao hazijarekodiwa wanapaswa kutoa ikiwa wana watoto wanaostahiki mpango wa Medicaid?

Wazazi wanaotuma maombi kwa niaba ya watoto wao wanaostahiki wanahitaji kutoa majina ya wanafamilia wote katika kaya zao, anwani zao za barua pepe, stakabadhi za uthibitisho wowote wa mapato yoyote na stakabadhi za uthibitisho wa ukaaji wa jimbo kutoka kwa mzazi/wazazi ili kubaini ustahiki wa mtoto pamoja na fomu ya maombi iliyotiwa sahihi. Wazazi hawahitaji kutoa maelezo ya uhamiaji au nambari ya ustawi wa jamii yao wenyewe ikiwa hawajitumii maombi kwa mpango wa Medicaid. Mpango wa Medicaid hautoi taarifa yoyote kwa asasi za kutekeleza sheria au Idara ya ICE.

### Je, watu walio na Kibali cha Muda cha Kuishi Marekani kutokana na Changamoto Nchini Mwao (TPS) wanaweza kutuma maombi kwa mpango wa Medicaid?

Hapana, watu walio na kibali cha TPS hawawezi kutuma maombi ya kuandikishwa kwa bima kamili ya afya kupitia mpango wa Medicaid. Hata hivyo, wanaweza kustahiki mpango wa Medicaid wa kugharamia hali ya dharura ilmradi tu wanatimiza masharti ya viwango vya mapato na masharti ya ustahiki wa ukaaji katika jimbo la North Carolina. Wanawake wajawazito na watoto walio na umri wa chini ya miaka 19 walio na kibali cha TPS wanastahiki kutuma maombi kwa mpango wa Medicaid ikiwa wanatimiza masharti mengine yote ya ustahiki na hawako chini ya kipindi cha kungoja cha muda wa miaka mitano. Watu walio na kibali cha TPS wanaweza kutuma maombi ya kujiandikisha kwa bima na kusaidia kulipia bima chini ya mpango wa Health Care Marketplace (ACA).

### Je, wapokeaji wa Sera ya uhamiaji ya Marekani ambayo inaruhusu wahamiaji fulani wasio na hati ambao waliingia nchini wakiwa watoto kukaa Marekani kwa muda na kuepuka kurudishwa nchi zao (Deferred Action for Childhood Arrivals, DACA) wanaweza kupataMedicaid?

Hapana. Chini ya sheria zilizotolewa na Centers for Medicare and Medicaid Services (CMS), watu walio na hali ya kuwa wafaidi wa Sera ya uhamiaji ya Marekani ambayo inaruhusu wahamiaji fulani wasio na hati ambao waliingia nchini wakiwa watoto kukaa Marekani kwa muda na kuepuka kurudishwa nchi zao hawachukuliwi kuwa wako nchini kihalali kwa madhumuni ya ustahiki wa bima huduma ya afya. Watu walio na DACA wanastahiki bima ya kugharamia huduma za hali ya dharura za Medicaid inapohitajika.

### Je, wafanyakazi wa shamba walio na viza ya H-2A wanastahiki bima ya mpango wa Medicaid?

Wakulima walio na stakabadhi zinazoonyesha hali za wao kuwa nchini kisheria wanaweza kustahiki ikiwa ni mwanamke mjamzito au mtoto aliye chini ya umri wa miaka 19. Watu wengine wote wanastahiki kupokea huduma za hali ya dharura za mpango wa Medicaid. Watu walio na viza ya H-2A wanaweza kutuma maombi ya kujiandikisha kwa bima na kusaidia kulipia bima chini ya mpango wa Health Care Marketplace.

### Je, wamiliki wa viza ambao sio wahamiaji (ikiwa ni pamoja na mwanafunzi, mtalii, wamiliki wa viza ya kazi, wamiliki wa viza ya utoaji usaidizi kwa maafisa wa serikali katika Uchunguzi wa uhalifu (U) na wengine wengi) wanastahiki mpango wa Medicaid?

Wanaweza kustahiki na kuondolewa kwenye kategoria ya watu wanaoongoja miaka mitano ikiwa hao ni wanawake wajamzito au watoto walio chini ya umri wa miaka 19. Watu wazima wasio wajawazito na walio na umri wa miaka 19 na zaidi wanastahiki huduma za hali ya dharura za mpango wa Medicaid pekee. Watu wanaotuma maombi kwa ajili ya kupata huduma za hali ya dharura pekee hawahitajiki kutoa hati za kuonyesha hali ya uhamiaji. Watu walio na viza zisizo za wahamiaji ambao ni wakazi wa North Carolina wanaweza kutuma maombi ya kujiandikisha kwa bima na kusaidia kulipia bima chini ya mpango wa Health Care Marketplace.

### Je, unahitaji usaidizi? Ratibu miadi ya kujiandikisha bila malipo na Mwelekezi mahiri.

Miadi inaweza kuratibiwa mtandaoni katika https://ncnavigator.net/schedule-online au kwa njia ya simu kwa 1-855-733-3711. Vielelezo vinaweza kusaidia katikae utumaji wa maombi kwenye mipango yote miwili ya Health Care Marketplace na Medicaid na huduma zinapatikana katika lugha 20+.

**Kwa maelezo zaidi, tembelea Medicaid.nc.gov/immigration.**



NC DEPARTMENT OF HEALTH AND HUMAN SERVICES